



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

MKOA WA KILIMANJARO
Mtendaji,

Ofisi ya Mkurugenzi

Halmashauri ya Wilaya

Simu : 27-2758441

ya Hai,

S.L.P 27,
HAI.

Fax : 27- 2757039

Barua Pepe: ded@haidc.go.tz

Kumb.Na. LG/MMH/30/2/21/065


KWA WANANCHI WOTE:

TANGAZO LA KUGAWA MAENEO YA UJENZI WA MADUKA YA BIASHARA

Mkurugenzi mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Hai anapenda kuwatangazia Wananchi wote kwamba,

1. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inakusudia kugawa maeneo ya kujenga maduka ya biashara kuzunguka soko la Gezaulole;
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inapenda kuwaalika watu binafsi, Ushirika, Makampuni, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo wa kujenga maduka kwenye eneo hilo kutuma maombi;

3. Mwombaji anapaswa kuwasilisha ombi kwa **KUJAZA FOMU** akiambatanisha na stakabadhi ya Malipo ya Tshs. 20,000/= kama ada ya maombi, ambayo haitarudishwa (non-refundable fee);
4. Fomu za Maombi zinapatikana **Ofisi ya Mapato na utapewa Control number ya kulipia ada ya fomu.**
5. Moja ya sharti kwa mwombaji ni kuhakikisha ananza ujenzi na kumaliza ndani ya siku 90 kuanzia siku anapokabidhiwa eneo la ujenzi wa Duka lake;
6. Maombi ambayo yatachelewa kwa muda uliopangwa hayatapokelewa;
7. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya Jumatatu, tarehe 31/05/2021, saa 9.30 Alasiri, na waombaji watakaopewa nafasi watatarifiwa kabla ya tarehe 09.06.2021.
8. Halmashauri ya Wilaya ya Hai haitalazimika kumkubali mwombaji yeyote kwa misingi ya upendeleo.
9. Mwombaji haruhusiwi kuomba eneo la ujenzi zaidi ya moja, mtu mmoja duka moja ili kutoa fursa kwa Wananchi wengine kupata nafasi.



Yohana E. Sintoo

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HAI
MKURUGENZI MTENDAJI W.
HAI

Limetolewa tarehe 10.05.2021